Ushirikishwaji ni ushiriki?

Jishindie kompyuta ndani!

Kijitabu hiki kimetayarishwa na watendaji wa Tamasha kwa kushirikiana na Twaweza

Waandishi:
Richard Mabala na Winston Churchill Shauri

Mchoraji:
Daniel Mzena

Wahariri:
Rakesh Rajani, Evarist Kamwaga, Joseph Ngwegwe na Justice Rutenge

Usanifu:
Winston Churchill Shauri

©Tamasha/Twaweza 2012

Barua: S.L.P. 15044, Arusha, Tanzania
Simu: +255 719 751 928
+255 787 220 233

Barua pepe: rmabala@yahoo.com
wchachi@yahoo.com

Tovuti: www.tamashavijana.org

Unaruhusiwa kunakili sehemu yoyote ya kijitabu hiki kwa sababu zisizo za kibiashara tu. Unachotakiwa kufanya ni kunakili chanzo cha sehemu uliyonakilia na kutuma nakala mbili kwa Tamasha.

Utangulizi

Ndugu wasomaji,

Vijana wanataka na wanatakiwa kushiriki katika ujenzi wa taifa letu. Tatizo ni kwamba mara nyingi 'wanashirikishwa', yaani, mipango hubuniwa na kupangwa na wazee. Kazi ya vijana ni kutekeleza tu yaliyoamuliwa. Hawana nafasi ya kuchangia mawazo, uchambuzi na ubunifu wao katika kuamua nini cha kufanya au jinsi ya kufanya. Kwa mujibu wa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana ya mwaka 2007:

"Vijana ambao ni takriban 65% ya nguvukazi na 35% ya wananchi wote hawawakilishwi katika maeneo mbalimbali na hawashiriki katika vyombo vya kufanyia uamuzi. Matokeo yake ni kwamba maamuzi yaliyo mengi hayazingatii matakwa ya vijana."

Katika utafiti uliofanywa na TAMASHA katika baadhi ya wilaya, vijana walilalamika sana kwamba hawapewi nafasi ya kushiriki, huku wazee wakidai kwamba vijana hawana kitu cha kuchangia. Hali hii huonekana mbaya zaidi upande wa wasichana ambao wanashiriki kidogo zaidi katika mikutano na hawasikilizwi kabisa.

Aidha, licha ya pendekezo la Sera ya vijana kwamba ushiriki urasimishwe kwenye maeneo yote yanayowahusu vijana, viongozi wa jamii walilalamika kwamba:

Hakuna miongozo ya kuwasaidia vijana waweze kushiriki katika vyombo vya kufanya maamuzi, labda kwa kupitia kamati mbalimbali.

Hivyo kila jamii imeachwa kujiamulia kuwashirikisha vijana au la. Lakini sehemu ambazo walipewa nafasi za kushiriki walitumia nafasi hizi vizuri sana

Vipi hali ya ushiriki ya vijana katika jamii yetu?

Richard Mabala
Mkurugenzi, Tamasha

Wahusika

Bonge: Mjasiriamali, mchambuzi wa mambo na mkereketwa wa maendeleo

Bibiye: Mwelimishaji rika, mchambuzi na mwanaharakati

Mwenyekiti: Kiongozi anayesikiliza na kuheshimu vijana. Mpenda maendeleo lakini anaamini zaidi msaada kutoka nje kuliko nguvu ya wananchi

Mtendaji: Mchapakazi lakini mrasimu. Hapendi vijana na azma yao ya kuchukua hatua wenyewe

Mwanakijiji Baba wa kijana mwelimishaji rika. Anatoa ardhi kwa ajili ya vijana kujenga kituo chao

Wawezeshaji rika wako kempu ya vijana

Hapana sisi ni vijana kama nyie.
Ah wapi! Nyie wote mambo safi.
Lakini sista hizi stadi za maisha zitatusaidia nini?

Zinatupa mwelekeo katika maisha. Kwa mfano kupanga malengo.
Malengo wapi? Wazee noma. Hawataki maendeleo yetu.
Malengo bila ajira yatasaidia nini?

Sawa. Lakini tumejaribu kufanya nini sisi wenyewe? Au tunalalamika tu?
We sista, baba anauza mashamba mimi nipate kazi wapi?
Na kijijini wanataka mikono yetu tu, akili hapana.

Una maana gani?
Kazi zote za kijiji wana-tutegemea sisi tu!
Lakini tukitaka kutoa wazo, nuksi. Hata kuchapwa twachapwa!

Ndio maana lazima tujipange. Tuwe na schemu yetu. Tutapigania maendeleo yetu.
Hakuna lolote bwana, bila msaada hawezi ntu kitu.
Kata zingine wamepiga hatua kweli na kituo chao. Na sisi tujenge cha kwetu.

Kwani inawasaidia nini?
Wale vijana wanapanga mambo yao. Na wana-tambulika! Shughuli zote zinawezekana.
Kwani kituo ni zaidi ya kempu? Bora tujichokee hapahapa tu!
Haya jamani, karibuni lakini. Tutajenga kituo chetu mtaona.

Wawezeshaji wanaondoka

Wanakutana na vijana wenzao
Tumeshaandaa vifaa na kesho tutaanza kufyatua matofali.
Hawa pia watakuwa pamoja nasi. Au?
Karibuni sana.

Lakini tukishajenga tutapata wapi vifaa na mambo mengine?
Tukijenga wenyewe, lazima wengine watatupiga tafu. Kuna asasi kibao.
Na idara ya maendeleo ya jamii pia.
Hamjidanganyi kweli nyie?

Ghafla tarishi wa kijiji anafika
Mnafanya nini hapa? Vijana wote mliagizwa kulima barabara yetu.
Kwa uamuzi wa nani? Mlitushirikisha saa ngapi?
Ohooo! Ngoja nimwambie mwenyekiti.

Yaleyale! Wazee noma! Vijana hatuna kitu.
Ndiyo maana lazima tujipange.
Twendeni tuwawahi.

Wenzenu wako wapi?
OFISI YA KIJIJI
Wanalima barabara. Tumegawana kazi.

Ina maana kazi yenu ni muhimu kuliko maendeleo ya kijiji?
Hata kazi zetu ni muhimu.
Maendeleo ya vijana ni maendeleo ya kijiji.

Mlitakiwa kuandaa ngonjera na wimbo kwa ajili ya ujio wa mbunge.
Wapi tulijadili?
Mkutanoni.
Hata tukija mkutanoni, hamtaki kutusikiliza.

Nyie vijana, wazee tukiamua, ni kazi yenu kutekeleza. Ujeuri huo mnapata wapi?
Sio ujeuri. Tunataka kuchangia hamtaki mchango wetu.
Basi tutaandaa ngonjera akija kituoni kwetu. Ataona mfano mzuri wa maendeleo.

Kituo!? Nani kawaruhusu? mmepata wapi kiwanja?
Baba yangu katupatia.
Mtaweza wapi? kempu nyingine tu hiyo!

We mzee usitudharau. Kwani sisi tuliwaambia mlewe hadi mnauza mashamba?
Basi basi. Si bora uje uone.
Haya twende. Kama si hadithi za alinacha.

Njiani
Hivi kweli umewapa vijana kiwanja?
Ndiyo. Lazima tuwawezeshe vijana kupata maisha.
Utakufa maskini wewe.


Sasa hiki kituo ni kwa ajili ya nini?
Si bure. Kuna mtu anawachochea siasa chafu!

Kituo hakina chama. Ni mali ya kila kijana kijijini.
Tutaanzisha miradi ya ujasiriamali na elimu rika.
Tutawafundisha vijana haki zao na wajibu wao washiriki kikamilifu.

Bila kusahau michezo na burudani.
Na kufanya mpango wa ulinzi wa wasichana wasinyanyaswe.
Na tutachagua viongozi wetu wenyewe watuwakilishe.

Mbona mnapanga wenyewe? Lazima ipitishwe kwa serikali ya kijiji na kata.
Kwa nini? kila kitu kwenu tu, Hatuvunji sheria. Na tunachangia maendeleo.
Ni vizuri. Tuletee maelezo hakuna shida.

Baada ya wiki moja.
Vijana mnajitahidi.
Asante mheshimiwa. Bila shaka mtatukumbuka na mfuko wa maendeleo ya jimbo. Tutafanya mengi zaidi.

Huu wimbo ushiriki, kuuimba hamchoki, mtazidi kula dhiki, kama tusemayo hamtaki,
Mbona mwafunika jua, kwa kipande cha kaniki,
tunataka - kuamua, na nafasi kushiriki
Vijana wanaweza mengi kwa nini tumewadharau?

Je wajua?

1. Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana inasema vijana ni watu wenye umri kati ya miaka 15 na 35 ingawa, katika jamii nyingi, mtu wa miaka 35 ni mtu mzima kabisa.
2. Vijana wanajisikia kudharauliwa na jamii zao. Mawazo yao hayathaminiwi wakichangia kwenye mkutano. Sehemu nyingine wanachapwa viboko kwa kutoa wazo mbadala.
3. MKUKUTA 2 ilitambua kwamba:

   Takriban 53% ya wananchi wanashiriki katika mikutano ya kijiji ingawa ni kikao muhimu sana cha kufanya maamuzi.

   Sehemu nyingi ni kwa sababu vijana wamesusa. *Vijana hawaoni umuhimu wa kushiriki katika mikutano maana hawasikilizwi na hawana uwezo wa kufanya maamuzi kwa mambo yao.* - Vijana, Iringa[1]
4. Wawezeshaji rika katika jamii nyingi sana wameonyesha vijana wanaweza kufanya nini wakipewa nafasi. Mkakati wa kupambana na UKIMWI usingefanikiwa bila wao.
5. Vijana wakipewa fursa ya kushiriki wanaitumia kikamilifu, ama kwenye jamii zao ama kwenye ngazi ya wilaya kupitia kwa mitandao yao ya vijana. Hii imewawezesha kupata ajira pia katika kutekeleza mipango ya halmashauri au asasi za raia waliotambua uwezo wao.
6. Ingawa kujitolea ni jambo muhimu, huwa maamuzi hayazingatii shughuli au nafasi zao. Ndiyo maana ni muhimu vijana washiriki katika maamuzi na mipango si tu katika utekelezaji.
7. Kituo cha vijana kinaweza kuwa kitovu cha maendeleo yao, kimafunzo, kimichezo na kijasiriamali pamoja na kushiriki.

1 Utafiti wa Tamasha

Tufanye nini?

Kwanza tuwaulize vijana wenyewe nini kifanyike. Vinginevyo tutakuwa tunawashirikisha tena badala ya kuwawezesha kushiriki. Lakini ili kuleta ushiriki wa vijana zaidi, inawezekana:

- Kuwawezesha kupata au kujenga kituo cha vijana iwe mali yao kisha kuwawezesha wapate vifaa na mbinu za kujitegemea.
- Vijana kuanzisha vikundi vyao vya uzalishaji.
- Kufuatilia mifuko ya vijana iliyopo kwenye wilaya. Katika salamu zake za mwaka 2012, Mhe Rais alisisitiza kwamba kila mkoa ulipewa shilingi bilioni moja kwa ajili ya wanawake na vijana.
- Kumshawishi Mhe. Mbunge kutoa kipaumbele kwa vijana katika Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo.
- Kuweka utaratibu wa uwakilishi rasmi ya vijana katika vikao vyote vya jamii na vya kata.
- Kushawishi uundaji wa vikundi vya wasichana ndani ya kituo cha vijana ili wasichana nao wapate uzoefu wa uongozi na kuongea hadharani.

Shindano

Toa maoni, jishindie kompyuta!

Ndugu msomaji, hivi karibuni Serikali ya Tanzania imeahidi kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi.

Kupitia mpango huu, Serikali inataka kukusikia.

Toa maoni yako kuhusiana na upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii; maji, elimu na afya.

Tuambie wazo moja kuboresha elimu, afya au maji. Halafu, tuambie mwananchi afanye nini kuleta mabadiliko.

Kila baada ya miezi mitatu kwa mwaka 2013, maoni kumi bora yatachaguliwa na kila shule itakayotoa washindi itapatiwa kompyuta ndogo mbili (laptops). Pia, maoni ya washindi yatachapishwa kwenye vitabu na tovuti.

Sharti: Kila mtu anaweza kutuma maoni, lakini zawadi zitatolewa kwa watakaondika *kupitia* shule zao tu.

Tuma maoni yako kabla ya tarehe 1 Novemba, 2013

Anuani: OGP Tanzania, S.L.P 38342, Dar es Salaam

Barua pepe: unasemaje@gmail.com

Kumbuka kuweka taarifa hizi:

- Tarehe
- Majina kamili, umri wako, jina la shule; jinsia (me/ke)
- Anuani kamili: SLP na makazi (kata, wilaya na mkoa); namba ya simu; barua pepe

Mpango wa Kimataifa wa Kuendesha Shughuli za Serikali kwa Uwazi **(Open Government Partnership - OGP).**

Open Government Partnership

Mpango wa OGP unahimiza shughuli za Serikali ziendeshwe kwa uwazi zaidi ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi, mwitikio wa Serikali, kupambana na rushwa na kujenga kuaminika zaidi. Twaweza inashirikiana na Serikali kuendeleza uwazi na ushiriki wa wananchi kupitia Mpango wa OGP.